

**P1 KISWAHILI**  
**KARATASI 1**  
**PTE**  
**MACHI/APRILI 2019**  
**MUDA: SAA 2**  
**MAAGIZO**

1. *Mtihani huu una sehem: Insha, Ufahamu, Matumizi ya lugha na sajili za lugha.*
2. *Ni muhimu sana ufuate maagizo uliyopewa mwanzoni mwa kila sehemu.*

**KWAMATUMIZI YA MTAHINI**

SEHEMU	SWALI	UPEO	ALAMA
1	1	20	
2	2	20	
3	3	30	
	4	20	
4	5	10	
JUMLA			

**SEHEMU YA KWANZA – INSHA (ALAMA 20)**

1. Andika insha isiyopungua maneno 350 kuhusu mojawapo ya mada zifuatazo
  - a) Wewe ni mwalimu mkuu wa shule ya vijiji. Andika mazungumzo kati yako na chifu wa kata kuhusu swali la wasichana kupachikwa mimba kiholele na kuozwa kwa wachumba wa lazima
  - b) Umuhimu wa kuhusisha jimii katika miradi ya maendeleo katika maeneo bunge
  - c) Malizia dondo hili, Niliamini kweli kuwa mwana wa mtu hulima na wa nyani hula kwa neema
  - d) Umoja ni nguvu utengano ni udhaifu

**2. SEHEMU YA PILI: UFAHAMU (Alama 20)**

**Soma habari ifuatayo kisha ujibu maswali**

Kwa kweli chakula ni muhimu sana kuimarisha mwili wa binadamu katika awamu zote za maisha kuanzia utotonii, ujanani, utu uzima na uzee wake. Kwa nujibu wa wanasyansi wakati mama mtoto anatunga mimba, anastahili kuanza kuimarisha hali yake ya lishe bora ili kijusi tumboni kianze kunawiri kiafya.

Uzee uwasilipo, mambo huanza kumwenda mhusika segemnege. Baadhi ya matatizo humkabili kila mmoja wa wazee kutegemea mazingira ya kuelewa kwake na chakula alichozoea maishani mwake. Wengine huonekana wakongwe zaidi wakiwa na umri wa miaka arubaini ilhali wengine wakaonekana vijana wakiwa na umri wa miaka sabini.

Dalili za kuingia kwa uzee hujidhihirisha katika mambo kadha ambapo ufanyakazi wa viungo mbalimbali nya mwili huanza kufifia ikiwemo misuli. Mhusika aliyekuwa akitimua mbio hapo awali hugeuza mwendo wake ukawa polepole mithili ya kinyonga au kobe. Mzee huyu hushindwa hata kuinia miguu yake anapotembea. Akipita nyasini utadhani ni njia aliyofunguliwa na joka linalonyinyirika kupita eneo lilo hilo siku nenda siku rudi kwake na kurejea mawindoni.

Ngozi ni kitu kingine kinachonyauka na kualegea kwa mtu aliyezeeka. Utapata nyamanyama zilizounda miviringo na mitararo zinaning'inia ovyo. Kwa wale wenye miili mikubwa hali huzidi kinyume na wenye miili midogo. Wazee hawa ambaa baadhi yao waliokuwa na sura tanashati, sasa wakicheka ni kana kwamba wanalia huku midomop yao ikiwa inaambia anayeiona, "Tafadhali nishikilie nisidondoke". Hata mgongo uliokuwa wima sasa huwa umejipinda na kulazimu mhusika kutumia mguu wa tatu. Wengine huenda wakitetema ambapo wakati mwingine hawawezi hata kushika kikombe cha maji kwa njia imara.

Fauka na hayo, fizi za wazee hulegea na wakang'oka meno. Ndiyo sababu utapata wengi wa wazee ni vibogoyo. Wanapopewa nyama wao humeza vipande vidogovidogo walivyopewa pasi kutafuna. Wao huhitaji kupewa maini au vyakula vyororo ili waweze kula bila mng'ang'ano.

Si uwezo wa fizi pekee unaofilia bali hata ule wa kuona huzuka ambapo wanaweza kushindwa kuona si vitu nya mbali tu bali hata karibu. Kwa mfano mzee atapewa gazeti atalileta karibu sana huku amevaa mijiwani yenyen lensi nene kumwezesha kuona.

Pia uziwi kwa wazee huongezeka na kuwakosesha kusikia vizuri hali inayowapokonya uwezo wao kuchangia katika mijadala mbalimbali. Bila shaka baadhi ya wanasyansi wamevumbua baadhi ya vidude kukabiliana na tatizo hili kwa fanaka za kiwastani. Kunayo madude yanayopachikwa kwenye masikio yanayohusika ili kunasa sauti. Hata hivyo, waliotumia kifaa hiki hudai wakishakutumia masikio huwauma sana. Wanasyansi bingwa wa chuo kikuu cha Harvad London, uigereza wamefanikiwa kutengeneze chembechembe muhimu zinazoweza kupandikizwa kwenye masikio hasa ya watoto wadogo kuwawezesha kusikia ambapo kwa wazee wenye umri kama wa miaka sitini na tano itakuwa vigumu kuwarejeshea hali yao.

Baadhi ya wazee hutokwa na mkojo ovyoovyo kwa vile ile misuli ya kushikilia au kuzuia isitoke huwa imeisha nguvu. Uwezo wa kufanya mahada pia hupungua mionganii mwa wazee ambapo haiwezi kuwa kama ilivyokuwa hapo awali. Tuseme kila kitu mwilini hudhoofika. Hata ule uwezo wa kuonja, kuguswa na kunusa hutoweka na wakati.

Ni kawaida katika baadhi ya maeneo hapa Afrika wazee kupatikana wameachwa kule vijijini hawana mbele wala nyuma. Wengine huanikwa na kuanuliwa kama mtama na si ajabu kupata

wengine wakinyeshewa na mvua iwapo watakosa uwezo wa kusota mwenyewe kurudi nyumbani. Wengine hufilia nyumbani bila yelete wa kuwajali. Angaa katika chi zilizostawi kimaendeleo zimeanzisha makao ya wazee ambapo wao hutunzwa kwa kuvishw, kulishwa mionganoni mwa mahitaji mengine.

Umfika wakati ambapo nchi zetu za Afrika zinatafaa kulioa jambo hili kipaumbele ili fedha fulani zitengewe mashaibu na ajuza wote ili kuwarahisishia maisha katika ulimwengu wa sasa. Aidha, swala la lishe bora lishugulikiwe kwa kuelimisha wahusika kuhusu umuhimu wa chakula bora. Hatua hii itapunguza baadhi ya shida zinazoambatana na kukosa lishe bora. Tukingojea eti kutafuta msaada kwa dawa za kupunguza uzee, ngozi bandika na kemikali nyinginezo bila jambo hili la kimsingi, tutakuwa tunamaliza muda na pesa bure!

Maswali

- a) Ipe taarifa hii kichwa mwafaka (al. 1)

---

- b) Ni jambo lipi la kimsingi ambalo linatafaa kuzingatiwa mapema ili kuepusha baadhi ya matatizo yanayoambatana na uzee (al.2)

---

- c) Mwendo wa mzee umesema kuwa hufifia umri unapozidi kwa kulinganishwa na viumbani gani? (al.2)

---

- d) Taja uwezo mbalimbali katika taarifa ambao mzee hupoteza kadiri umri unavyoongezeka (al.5)

---

- e) Taja makundi mawili yaliyotajwa katika habari hii na juhudini wanazofanya kukabiliana na matatizo yanayokabili watu uzeeni (al.2)

---

- f) Eleza maana ya maneno yafuatayo jinsi yaliviyotumika katika ufahamu (al. 4)
  - (i) Kijusi \_\_\_\_\_
  - (ii) Kunyinyirika \_\_\_\_\_
  - (iii) Tafadhali nishikilie nisidondoke \_\_\_\_\_
  - (iv) Kusota \_\_\_\_\_

---

- g) Je, unaafikiana na hatua ya kuwashhughulikia wazee? Ungechukua hatua zipi? (al.4)

---

3. SEHEMU YA TATU – MATUMIZI YA LUGHA (ALAMA 50)
- a) Tunga sentensi mbili kuonyesha matumizi tofauti ya kiambishi ki (al.2)
- b) Badilisha vivumishi vifuatavyo viwe vitenzi (al.2)
- (i) Bora \_\_\_\_\_
- (ii) Tukufu \_\_\_\_\_
- c) Tumia neno zuri katika sentensi moja kama (al.2)
- (i) Kivumishi \_\_\_\_\_
- (ii) Kielezi \_\_\_\_\_
- d) Tunga sentensi yenye. Muundo ufuatao; Nomino ya jamii + kihuishi + kitenzi kishirikishi+ kielezi cha mahali (al4).
- e) Andika kwa ukubwa (al. 2)
- Ngoma ikipigwa sana inapasuka
- f) Andika maana mbili zinazojitokeza katika sentensi hii (al. 2)
- Alimwonea juma
- g) Andika tofauti mbili kati ya sauti /p/na/f/ (al.2)
- h) Maneno haya yako katika ngeli gani? (al.2)
- (i) Marashi \_\_\_\_\_
- (ii) juma \_\_\_\_\_
- i) Andika sentensi ifuatayo kwa wingi (al.2)
- Uteo ulionunuliwa na mchuuzi yule umepotea
- j) Changanua sentesi ifuatayo kwa kutumia matawi Wale wenye uzembe hawatapasi mtihani huu (al.4)
- k) Kanusha sentensi ifuatayo kwa wingi (al.2)
- Wewe utafeli mjarabu huu
- l) Tunga sentensi moja kutofoutisha maana ya faa na vaa (al.2)
- m) Nyambua vitenzi vifuatavyo kauli ya kutendesha (al.2)
- (i) La \_\_\_\_\_
4. Ruka \_\_\_\_\_
- (a) Andika sentensi hii upya ukitoa visawe vyta maneno yaliyopigwa mstari Msichana aliangukiwa na sera alipokuwa akiipanda. (al.3)

- (b) Sikio ni kwa kusikia; moyo ni kwa \_\_\_\_\_ (al.1)
- (c) Kapu la kubebba matunda huitwa \_\_\_\_\_ (al.1)
- (d) \_\_\_\_\_ ni ugonjwa wa kupooza mwili (al.1)
- (e) \_\_\_\_\_ ni vazi la kike linalofunika mwili kuanzia kiunoni hadi magoti (al.1)
- (f) Mnazi huzaa nazi na mpunga huzaa \_\_\_\_\_ (al.1)
- (g) Umati wa watu pia huitwa \_\_\_\_\_ (al.1)
- (h) Kishaufu huvaliwa wapi \_\_\_\_\_ (al.1)
- (i) Mtoto wa binadamu ni kingadu na mtoto wa kipepeo ni \_\_\_\_\_ (al.1)
- (j) Riba ni malipo gani \_\_\_\_\_ (al.1)
- (k) \_\_\_\_\_ ni mtu wa kuuza vitu kwa kuzitembeza (al.1)
- (l) Tegua kitendawili kifuatacho  
Ninapopiga mwanagu watu hucheza \_\_\_\_\_ (al.1)
- (m) Andika tarakimu 22,222,201 kwa maneno (al.1)

---

(n) Andika kinyume cha sentensi hii  
Mvulana mwembamba ameketi (al.2)

---

(o) Kamilisha methali ifuatayo  
\_\_\_\_\_ huingia mwenyewe (al.1)

(p) \_\_\_\_\_ ni mtu asiyeweza kusema ilhali \_\_\_\_\_ ni mtu  
aliyepofuka jicho (al.2)

SEHEMU YA NNE: SAJILI YA LUGHA (ALAMA 10)

5. Taja na ufanue sifa za sajili ya mahakama (al.10)
-